# UBASHIRI WA KCPE DARASA LA NANE 2023 KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Nikiwa shuleni hakuna somo __1__ zaidi __2__ la Kiswahili. __3__ nilikuwa karibu __4__ baada ya kukosa kutofautisha viambishi. Mwalimu alinihitaji kutambua viambishi vya __5__ 'mtalimiana.' Baada ya kulemewa mwalimu aliniambia jibu sahihi lilikuwa __6__. Hapo nikakumbuka kuwa tangu awali __7__ kuwa mja hawezi kubadili __8__ maisha yake, hata akajitahidi vipi.

1. A. niliyoenzi B. nilioenzi C. nililoenzi D. nilizoenzi
2. A. kuliliko B. kuliko C. kuiliko D. kulichoko
3. A. Vilevile B. Aidha C. Licha ya D. Hata hivyo
4. A. kwenda nguu B. kwenda mrisi C. kwenda pecha D. kwenda njongwanjogwa
5. A. nomino B. kitenzi C. kiwakilishi D. kiunganishi
6. A. ian-a B. m-ta-lim C. lim-ian-a D. i-a-na
7. A. ningekuwa nimeamini B. nikiwa nimeamini C. ninakuwa nimeamini D. nilikuwa nimeamini
8. A. mwelekeo ya B. mkondo wa C. dira wa D. mustakabali ya

Mawazo yangu yalipigwa jeki na methali __9__. __10__ kwamba hayo yalikuwa __11__ yangu na hakuna vile ningetambua viambishi vyovyote. Mwalimu wa Kiswahili __12__ kutoka kwenye usingizi huo. Alinionya __13__ __14__ huku nikisingizia mapenzi ya Mungu. Alitaka nielewe kuwa mimi __15__ nahodha wa maisha yangu.

9. A. jitihada haiondoi kudura. B. penye nia pana njia C. dhamira ni dira D. mtaka la waridi sharti adhurike
10. A. Nilishika B. Nilishikika C. Nilishikizia D. Nilishikilia
11. A. mapenzi B. majaliwa C. matilaba D. manufaa
12. A. ndio alinizindua B. ndivyo alivyonizindua C. ndiwe aliyenizindua D. ndiye aliyenizindua
13. A. mithili ya B. baina ya C. dhidi ya D. juu ya
14. A. kuwa kupe B. kuwa pweza C. kuwa mbumbumbu D. kuwa jeta
15. A. ndiye B. ndio C. ndimi D. ndiwe

Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi.

**16.** ***Chagua ukanusho wa:***
Kiranja alichaguliwa kwani alikuwa amehitimu.
A. Kiranja hajachaguliwa kwani hakuwa amehitimu.
B. Kiranja hakuchaguliwa kwani hakuwa amehitimu.
C. Kiranja hakuchaguliwa kwani hajakua amehitimu.
D. Kiranja hajachaguliwa kwani hajakuwa amehitimu.

**17.** Ni jibu lipi lenye maneno ya aina moja.
A. Chupa, imba, inuliwa.
B. Jana, vibaya, chinja.
C. Salama, sahani, bilauri.
D. Mvivu, polepole, mnene.

**18.** Ni methali gani isiyolingana na nyingine hapa?
A. Zimwi likujualo halikuli likakumaliza.
B. Damu ni nzito kuliko maji.
C. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.
D. Isipowasha hunyeza.

**19.** Chagua jibu lenye kivumishi kilichoundwa kutokana na nomino.

| | | |
|---|---|---|
| A. Uaminifu | - | Mwaminifu |
| B. Cheka | - | Mcheshi |
| C. Legea | - | Ulegevu |
| D. Pona | - | Uponyaji |

**20.** ***Chagua kauli ya kutendewa ya:***
Tatu alichukua pete ya Zawadi.
A. Pete ya Zawadi ilichukuliwa na Tatu.
B. Pete ilichukuliwa Tatu kwa Zawadi.
C. Zawadi alichukuliwa pete na Tatu.
D. Zawadi alichukuliwa pete kwa Tatu.

**21.** ***Chagua sentensi ambayo itaunganisha sentensi zifuatazo:***
(i) Mgonjwa alienda hospitalini mapema sana.
(ii) Mgonjwa alitibiwa kabla ya wengine.
A. Minghairi ya mgonjwa kuenda hospitalini mapema sana, alitibiwa kabla ya wengine.
B. Mgonjwa alienda hospitalini mapema sana hivyo basi alitibiwa kabla ya wengine.
C. Mgonjwa aliendá hospitalini mapema sana ilhali alitibiwa kabla ya wengine.
D. Mgonjwa alienda hospitalini mapema sana licha ya kutibiwa kabla ya wengine.

**22.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi kimilikishi.
A. Msafiri wa nne alipata kibali lakini wale hawakupata.
B. Mfanyakazi wa tatu alistaafu lakini wengine walibakia.
C. Mtoto wao aliamka mapema lakini huyu alichelewa.
D. Mzazi wake alihudhuria sherehe lakini wangu hakuhudhuria.

**23.** Ni sentensi ipi iliyotumia wakati uliopita hali timilifu?
A. Ngao hii itakuwa imetumika kabla ya mashindano ya mwakani.
B. Ngoma ile ilikuwa imepasuliwa baada ya wachezaji kupumzika.
C. Nguo yake ilikuwa inanunuliwa kabla ya sherehe hiyo.
D. Nyumba yao itakuwa inajengwa baada ya kubomolewa.

**24.** Bainisha sentensi iliyotumia kiambishi <u>-ka-</u> kuonyesha amri.
A. Mpishi aliandaa chakula akakipakua.
B. Nenda ukanawe mikono vyema!
C. Mlango umefungika vizuri.
D. Alienda hospitalini akamwone mgonjwa.

**25.** ***Tambua maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo.***
Fahali <u>yule</u> alimshambulia kijana aliyepita <u>karibu na</u> zizi hilo.
A. Kiwakilishi, kivumishi
B. Kivumishi, kiunganishi
C. Kivumishi, kiwakilishi
D. Kivumishi, kihusishi

**26.** Chagua sentensi isiyo sahihi kisarufi.
A. Majadume wale wenye miraba minne ni hodari.
B. Mwimbaji mwenye kufurahisha ni yule.
C. Mgonjwa mdhaifu ametibiwa leo.
D. Popote pale penye miti panavutia mno.



Compiled and distributed by schools Net Kenya | Place your order online via the website | Mob. 0734579299 |
Email: ordersnkenya@gmail.com Website: www.schoolsnetkenya.com

Rais amesema kuwa ni jukumu la kila mtu kuhakikisha kuwa usalama umedumishwa nchini mwetu. *Kulingana na taarifa aliyopokea* baada ya kuunda kamati ya kuchunguza viini vya ukosefu wa usalama nchini, rais amesema kuwa kuna vikundi mbalimbali vinavyotekeleza uvamizi dhidi ya wananchi. Akizungumza na wanahabari nje ya ikulu, rais alisema kuwa serikali yake haiwezi kuvumilia usafirishwaji jongomeo wa raia wasiokuwa na hatia.

Kulingana na raisi, kuna sababu anuwai zinazosababisha kuwepo kwa ukosefu wa usalama nchini. Alisema kuwa kuna watu humu nchini waliojawa na tamaa na ubinafsi. Watu hawa huwatumia vijana kutekeleza mavamizi nchini kwa lengo la kujifaidi kisiasa na hata kirasilimali. Alisema kuwa mavamizi hasa yale yanayohusiana na vita vya kikabila yametokana na uroho wa wanasiasa. Umero huu umewafanya wahusika kuwachochea wananchi dhidi ya wenzao. Hali hii imewafanya watu wengi kufukuzwa wanakoishi.

Rais aliendelea kusema kuwa visa vya uhalifu vimekithiri nusura kuruka mipaka. Siku hizi ni muhali kwa jua kuzama pasipo kusikia habari nyingine za kuatua moyo kuhusu mauaji, ubakaji, wizi wa mabavu na dhuluma dhidi ya watoto. Mambo hayo yakipuuzwa huenda tukaishia kujenga ukuta baada ya kushindwa kuudhibiti ufa.

Kando na ugaidi maovu mengine yanayotisha sana wakati huu ni ulanguzi wa watu. Hii ni hali ambapo watu wanasafirishwa kisiri kutoka eneo moja hadi jingine kwa sababu mbalimbali. Ulanguzi huu unaweza kwa wa kutoka vijijini hadi mijini, nchi hadi nyingine au hata bara hadi jingine. Mara nyingi watu hawa hughilibiwa kuwa maisha ya kule wanakoelekea ni bora yaani, <u>waendako ni paradiso kunakonuka pesa</u>. Hata hivyo, wengi wao huishia kujiuma vidole mambo yanaposibu kuwa kinyume na matarajio.

Je, ulanguzi wa watoto huchangiwa na nini? Umaskini uliokithiri ni kichocheo kikuu cha hali hii. Wazazi wanawauza watoto wao kwa walanguzi wanaposhindwa kuwakimu. Wengine ni watu wazima ambao angaa hujipeana kwa hiari ili wapate njia ya kujitosheleza.



Compiled and distributed by schools Net Kenya | Place your order online via the website | Mob. 0734579299 | Email: ordersnkenya@gmail.com Website: www.schoolsnetkenya.com

Sababu nyingine kuu ni ukosefu wa elimu. Mtu aliye na elimu hujinyima nafasi nyingi za kujiendeleza kiuchumi. Huku kukosa nafasi huenda kukamtia kiu ya kutaka kujaribu kwingineko. Waajiri wanaotafuta vibarua wa kulipwa ujira wa kijungujiko nao huwa tayari kuwapokea watu wa aina hii kwa mikono miwili. Wengi wa wale wanaosafirishwa huishia kufanyishwa kazi za mtulinga bila kujali kuwa wengi wao huwa wangali watoto.

Mila na tamaduni za jamii aidha zinaeneza hali hii. Baadhi ya jamii huwachukulia watoto kama kitegauchumi. Si ajabu katika jamii hizi kuwaona watoto wakiuzwa au kutolewa wakatumikishwe huku wakisafirishwa bila hiari yao. Kwingineko hata biashara ya utumwa huchukuliwa kuwa shughuli halali katika jamii.

Kile ambacho ningetaka kieleweke hapa ni kuwa, ulanguzi huu wa watoto au watu una athari chungu nzima. Wahasiriwa hutenganishwa na jamaa zao huku wengine wakiachana wasikutane tena katika uhai wao. Kule walikoita kwao hubakitu katika msimulizi huku wakikumbuka walivyoacha usalama na mapenzi ya jamaa zao.

Kule wanakohamishiwa watu hawa husheheni dhiki za kila nui. Katika kutumikishwa kuna wale wanaopata majeraha mabaya. Wanapougua hata hawatafutiwi huduma za matibabu. Wapo wanaodhulumiwa kimapenzi na kutishiwa usalama wao wakithubutu kutoa taarifa kwa vyombo vya dola. Watu hawa huishi kwa hofu isiyo na kifani. Utu wao hudhalilishwa hata wakakosa hamu ya kuendelea kuishi.

Nao wale wanaodirika kukata minyororo na kuwa huru huwa wameshabadilika kabisa. Baadhi yao huingilia vitendo vya ukiukaji wa sheria kule ugenini. Wao hujiunga na magenge ya uporaji, ulanguzi wa dawa za kulevya, usherati na maovu mengine ya kijamii. Iwapo waathiriwa hawa wangesalia katika maeneo yao huenda wangekuwa na mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa maeneo yao.

Nia zikiwa moja kilicho mbali huja. Serikali inapaswa kukabiliana na ulanguzi wa watu kwa kutoa nafasi za elimu, kufungua njia mbalimbali kwa wananchi ili wajiendeleze kiuchumi na kuwakabili walanguzi ili wajulikane wazi na jamii. Wanajamii nao wakae ange kuwatambua walio na nia ya kujifaidi kwa njia haramu ya ulanguzi wa binadamu. Wakae wakijua siku za mwizi ni arubaini.

**31.** Ugaidi na utekajinyara:
A. Ni matukio ambayo yamezidi kuliongezea taifa letu huzuni.
B. Ni masuala mawili ambayo yamelipa taifa letu pasbau kubwa.
C. Ni masuala mawili ambayo yamelipa taifa na raia wake woga mwingi.
D. Ni masuala mawili makubwa yanayoipa serikali wasiwasi mkuu.

**32.** Wanaondeleza ugaidi,
A. ni watu ambao wanajulikana vyema na wanahabari wote.
B. hupata ufadhili wao kutoka kwa wanahabari wa idhaa kuu nchini.
C. si wageni wasiojulikana na raia husika.
D. wanawatishia raia husika ikiwa watawasema kwa vyombo vya dola nchini.

**33.** Madhara makuu zaidi ya ukosefu wa usalama kwa mujibu wa aya ya pili ni
A. watu kuhamishiwa wanakoteswa.
B. watu kupoteza maisha.
C. watu kupoteza mali ya mamilioni ya pesa.
D. watu kutenganishwa na jamaa zao kwa kuhamishwa wanakoishi.

**34.** Kulingana na aya ya nne, msimulizi anamaanisha nini kwa 'tukaishia, kujenga ukuta kwa kushindwa kuudhibiti ufa.'
A. Kukosa kutambua hatari hadi pale inapoinuka.
B. Kuanza kuharibikiwa mambo bila kuwa na tahadhari.
C. Mambo kuharibika kabisa kwa kukawia kutatua shida.
D. Kufanya ujenzi baada ya ukuta wa nyumba kuanguka.



Compiled and distributed by schools Net Kenya | Place your order online via the website | Mob. 0734579299 | Email: ordersnkenya@gmail.com Website: www.schoolsnetkenya.com

**35.** Kifungu hiki kinazungumzia ugaidi na
A. kutumia njia haramu kuwapeleka watu wa sehemu moja kwingine kwa hila.
B. kuwapa watu kazi kwa ujira wa kiwango cha chini.
C. tabia za kuwauzia watu dawa za kulevya.
D. kusafiri kwa binadamu kutoka eneo moja hadi jingine.

**36.** Gani si mojawapo ya sababu inayochangia ulanguzi wa binadamu?
A. Uhaba wa nafasi za kujiendeleza.
B. Ukosefu wa maarifa.
C. Ukosefu wa mahitaji muhimu.
D. Ajira za kifahari.

**37.** Kazi za mtulinga ni zile
A. zenye malipo ya chini ya bora mkono uende kinywani.
B. zinazohitaji nguvu nyingi.
C. za kulazimishwa bila hiari ya mtu.
D. za kupokezana kwa zamu.

**38.** Kifungu kinaonyesha kuwa
A. kuna wale wanajinasua kwenye dhiki wanazosababishiwa.
B. wanakopelekwa wale waliolanguliwa hupokelewa kwa njia ifaayo.
C. watu wengi hushiriki maovu kwa hiari yao.
D. hamu ya kuishi hupungua mtu anapojinasua kwa wakandamizaji.

**39.** Kifungu kimeonyesha wazi kuwa maovu katika jamii yatakabiliwa zaidi kwa njia ya
A. ujasiri
B. unyenyekevu
C. ushirikiano
D. imani

**40.** Taja tamathali mbili zinazojitokeza katika kauli hii:
***Waendako ni paradiso kunakonuka pesa.***
A. Istiari, kinaya
B. Istiari, chuku
C. Jazanda, ishara
D. Tashbihi, istiari

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50***

Baada ya kumaliza masomo yake Mlachake aliyoyomea jijini Nairobi kutafuta kazi. Alikuwa na bahatii kama mtende kwani alipata kismati cha kazi katika kiwanda kimoja cha kusindika mafuta. Lakini hakukaa sana hapo. Akafanya kazi kwa muda kisha akaondoka. "Mlachake bwana, mtu lazima utafute ustaarabu. Kukaa mahali pamoja sio ustaarabu unaweza kuota mizizi!" aliwaambia waliomdadisi.

Baada ya kutoka kampuni hiyo ya mafuta, Mlachake alipata kazi nyingine katika shirika la reli. Bila shaka Mlachake alikuwa na nyota ya jaha. Kazi yake mpya ilimwezesha kupata fursa ya kusafiri nchi nyingi ulimwenguni. "Ni vyema ukatembea uone dunia. Mtu hawezi kuishi palepale kama jiwe," alisema Bwana Mlachake. Mlachake alizuru nchi nyingi tangu Bukini, Ngazija, Omani hadi Ulaya. Hali yote ya kiuchumi ikapanda mithili ya tiara. Sasa akawa na mali nyingi.

Hata hivyo wakati Mlachake alikwea ngazi ya kiuchumi, hali ya wananchi wengi nchini iliendelea kuwa ya kuhuzunisha. Matatizo ya kiuchumi yalifanya vijana wengi waliohitimu masomo kukosa nafasi za kazi. Wengine waliokuwa na kazi hizo walifutwa kutokana na mipango mbalimbali ya kampuni ya kuyabana matumizi yao. Watu wengi walijikuta mitaani wakizunguka kutwa kuchwa bila ya kujua watakula nini wala watalala wapi. Wengine walijikuta wakijutia pesa walizozihariji siku za nyuma walipodhani wangekuwa kazini milele wakiongozwa na ile imani ya ponda raha kufa kwaja. Kwa wengi jua la maisha yao mazuri lilikuwa likielekea machweo. Lakini kwa upande wa Mlachake jua la ufanisi lilikuwa bado mawio.

Siku moja Mlachake akiwa kazini, alipata ajali. Shirika la reli likaweza kumlipa fidia. Hapo ndipo maisha ya Mlachake yalibadilika kabisa. Fidia aliyolipwa baada ya kuumia miguu aliisarifu vyema. Alijenga



Compiled and distributed by schools Net Kenya | Place your order online via the website | Mob. 0734579299 |
Email: ordersnkenya@gmail.com Website: www.schoolsnetkenya.com

bahari la nyumba kijijini na nyingine akaamua kuziweka akiba kwa nia ya kujiingiza kwenye siasa. "Ninataka kuingia bungeni, nisikilizwe kwenye redio mimi mwenyewe!" aliwaambia marafiki zake. Muda si muda habari zenyewe zikatangaa kijiji kizima kama pepo za chamchela. Baadhi ya watu walianza kumdhihaki kuwa hakuweza kumudu kampeni za uchaguzi ambazo zilikuwa na kukuru kakara nyingine.

Harakati za uchaguzi zilipokaribia. Mlachake alifanya maandalizi yake ya uchaguzi. Hata hivyo, watu walisema kuwa hakuwa na uwezo wowote kwa sababu hakuwa na pesa za kutosha. Mpinzani wake, Bwana Hela aliahidi kufanya kampeni ya kukata na shoka kuhakikisha kuwa ameuhifadhi ubunge wa eneo bunge hilo kwa takribani miaka ishirini, hakuwa ameleta maendeleo yoyote. Kila mara baada ya uchaguzi aliyoyomea mjini hadi uchaguzi mwingine ulipokaribia tena. Hakuna aliyemsikia kwa heri wala kwa shari. "Hata mimi sikumsikia kwenye kijiredio changu!" Mlachake aliwaambia watu.

Hata hivyo Bwana Hela naye alikuwa gwiji wa wajanja. Kila uchaguzi ulipokaribia alinunua magunia ya mahindi na kuyasambaza haraka haraka kwenye eneo bunge lake. Ilitokea sadfa kuwa mara nyingine kulikuwa na njaa kubwa wakati wa uchaguzi. Watu walipopata mahindi hayo walimpigia Hela kura naye akajisemea, "wajinga ndio waliwao."

Hata hivyo, mara hii Hela hakuwa na bahati maadamu hakukuwa na njaa hata kidogo. Mvua ya masika ilinyesha vyema waja wakavuna mazao ya kazole. "Mara hii ataniona. Ni mimi na yeye!" Alisema Mlachake. Ingawa watu hawakumthamini sana Mlachake, walimstahabu yeye kuliko Bwana Hela. Jinsi kampeni zilivyozidi kuendelea ndivyo ilivyoonekana wazi kuwa huenda Mlachake akaibuka mshindi. Bwana Hela alipotanabahi kuwa wapiga kura walikuwa wakimshabikia Mlachake, alipigwa na butwaa. Sasa angefanya nini ilhali watu hawakuwa na njaa? Ilibidi atafute mbinu mpya.

Siku mbili kabla ya uchaguzi, Bwana Hela aliwasili kutoka jiji kuu na magunia mawili yenye vifuko vilivyokuwa vimefungwa kama mchele au sukari. Aliwachukua vijana kadhaa akawakabidhi mifuko hiyo ili wawagawie wenzao walishirikiana nao kumpigia kampeni. Ndani ya vifuko hivyo mlikuwa na njugu. Adinasi walipogundua mipango yao wakawaambia, <u>"Sisi si watoto wa kughilibiwa kwa njugu, wapelekeeni watoto wa shule."</u>

Vijana wale walisikika wakisema, "Hizi si njugu za huku mashinani. Hizi huipa miili nguvu mpya kuweza kushiriki katika harakati za kampeni, ni uvumbuzi mpya wa kisayansi. Bwana Hela anataka tumfanyie kampeni kwa nguvu na msisimko ili akamilishe miradi aliyoianzisha," walisema. Vijana hawa wenyewe walikuwa wakizitumia njugu hizo na kusisimkwa ajabu.

Waliweza kuuponda wa fisi wakiimba nyimbo za kumsifu Bwana Hela na kuwahimiza watu wampigie kura. Uvumi ulienezwa kuwa njugu hizo ziliweza kutuliza akili na kulainisha viungo vya mwili ajabu. "Ah! Si mbaya kama zinawatia watu hamasa ya kutenda kazi, wakasema kwa furaha. Hawa waliwashawishi wenzao wengine na kuunda kundi sawa na la vijana waliompigia Bwana Hela debe kwa msisimko mkubwa.

Naye Mlachake alifanya juu chini akajipatia kifuko kimoja na kukihifadhi. Kama kawaida yake hakusombwa na wimbi la kuzijaribu njugu hizo. Siku ya uchaguzi ilipofika, Bwana Hela akashinda kwa mara nyingine. Wakati huo Mlachake alikuwa ameondoka kuelekea jiji kuu wengine wakituhumu alikuwa ameenda kufuatilia matokeo ya uchaguzi akishuku kuwa huenda walimrubuni. Hatimaye Mlachake aligundua kuwa zile njugu zilikuwa dawa za kulevya. Bwana Hela akatiwa nguvuni akisubiri kufunguliwa mashtaka. Watu walipigwa na butwaa.



Compiled and distributed by schools Net Kenya | Place your order online via the website | Mob. 0734579299 |
Email: ordersnkenya@gmail.com Website: www.schoolsnetkenya.com

41. Zifuatazo ni sifa za Mlachake ila
A. mwenye bidii
B. mwenye majitapo
C. mwenye ari
D. mwenye masimango

42. Tambua tamathali mbili zinazojitokeza katika kauli hii:
***Hali yake ya kiuchumi ikapanda mithili ya tiara.***
A. Tashhisi, tashbihi
B. Tashtiti, tashbihi
C. Kinaya, istiara
D. Chuku, tashbihi

43. Jua la ufanisi lilikuwa bado mawio. Hii ina maana ya kuwa
A. Mlachake alikuwa na ufanisi mkubwa akilinganishwa na wenzake.
B. Mlachake ndio sasa hali ya kiuchumi ilikuwa imeimarika zaidi.
C. Mlachake ndio sasa hali yake ya kiuchumi ilikuwa imedorora zaidi.
D. Mlachake alikuwa na fadhaiko la moyo kutokana na hali yake ya kiuchumi.

44. Kulingana na aya ya nne
A. waliomwumiza Mlachake mguu waliagizwa kumlipa faini.
B. Mlachake aliumia mguu alipokuwa akisafiri kwa reli.
C. Mlachake alikuwa na mpango bora katika matumizi ya kipato chake.
D. Kustaafu baada ya kuumia ndiko kulikompa Mlachake wazo la kuingilia siasa.

45. Ni wazi kuwa waliopuuza azma ya Mlachake ni wale ambao
A. waliamini kuwa uongozi humhitaji mtu awe na uwezo wa kiuchumi.
B. hawakukitambua kipawa chake cha uongozi.
C. walipuuza mchango wa waliohitimu katika uongozi.
D. walikuwa na uhakika kwamba hawezi kushinda katika uchaguzi.

46. Kulingana na aya ya saba, Bwana Hela hakuwa na bahati kwa sababu
A. Mlachake alikuwa mshindani mkali kuliko wale aliomenyana nao hapo awali.
B. Janga ambalo angetumia kujifaidi halikuwepo.
C. Wakazi wote walipuuza msaada wake licha ya tatizo lao.
D. Mvua ya masika ilikuwa ikinyesha wakati wa kupiga kura.

47. Si kweli kusema kwamba:
A. Bwana Hela hakuwa kiongozi mwadilifu.
B. Mlachake naye alikuwa na udhaifu wake.
C. Baadhi ya wakazi walimwona Bwana Hela kama kipenzi chao.
D. Kukosekana kwa njaa ndiko kulikowafanya watu wamchukie Mzee Hela.

48. "Sisi si watoto wa kughilibiwa kwa njugu, wapelekeeni watoto wa shule. Kauli hii inaonyesha wazi kuwa
A. wakazi wanaiona njia anayotumia Bwana Hela kuwapumbaza kama isiyoweza kumzalia matunda yoyote.
B. wakazi wameweka msimamo thabiti kumpigia Mlachake kura badala ya Bwana Hela.
C. wakazi wamezoea njugu bora kuliko zile za Bwana Hela.
D. wakazi wana uhakika kuwa watoto wao hudanganywa kwa njugu.

49. Busara ya Mlachake inaonekana pale
A. alienda mjini kufuatilia hesabu ya kura.
B. alitambua madhara ya njugu pindi tu alipoziona.
C. aliwashauri wakazi dhidi ya kutumia njugu za Bwana Hela.
D. alitumia mikakati ifaayo kukabili uhalifu wa Bwana Hela.

50. Kulingana na kifungu hiki, ni methali gani hailengi ujumbe wa kifungu hiki.
A. Siku za mwizi ni arubaini.
B. Pwagu hupata pwaguzi.
C. Ujanja wa nyani huishia jangwani.
D. Baada ya dhiki ni faraja.



Compiled and distributed by schools Net Kenya | Place your order online via the website | Mob. 0734579299 |
Email: ordersnkenya@gmail.com Website: www.schoolsnetkenya.com